Jiwe la kiroho la kujengea na.15

# KITAMBULISHO CHA KIUNGU

***Mt 24:27 Akaanzia kutoka Musa na manabii wote,akawaeleza katika maandiko yote mambo yalio mhusu Yesu mwenyewe.***

Sikiliza kile nabii wa Mungu alichosema kuhusu hilo: Yeye, Yesu alikuwa na imani na nguvu zake.Ni kwa namna gani? Alisema "Siwezi kufanya lolote mimi mwenyewe***"(Yohana 5:19)*** kwa nini? Alitegemea kile alichokuwa; Alitegemea ufahamu ya kwamba Yeye alikuwa Neno, na alikuwa na imani kwa Mungu [Neno] na lilikuwa ndani yake, na hilo lilimpa imani kwa sababu alitambua Nafasi yake. Alitambua kile alichokuwa kwa sababu maandiko yasema kile alichokuwa ***[Luka24:25-27;44-45].***Na hapo kila maandiko yalikubaliana,kuthibitisha kuwa yeye alikuwa hasa kile maandiko yalisema vile atakavyo kuwa,na alijua yeye ni nani.Kwahiyo alitegemea vile Mungu alivyo muumba yeye,na kama alifanya hivyo je hatuwezi kile Mungu alichotufanyia kama wa aminio?"Ishara hizi zitatufanya na wamini ***(Marko16:17-18)***Alikuwa na imani na kile alichokuwa.Na kama umwaminio,unaimani ya kile ulicho:wewe ni mwaminio! Na kama unaimani kwa Mungu, Biblia inasema hapo katika ***(1Yohana.3:20-22)"***ikiwa mioyo yetu inatuhukumu, basi hatuwezi kuwa na imani, lakini kama mioyo yetu haituhukumu, basi tuna imani tunauhakika na Mungu" Lakini kama unafanya vitu ambavyo sio sawa, huwezi kuwa na imani kwa Mungu.Sasa unaona unajisumbua tu (automatikii) kwamba uko makosani utajiweka mahali mwenye dhambi, kwa kutambua ya kuwa uliofanya makusudi. Lakini kama moyo wako haukuhukumu na unajua wewe ni mwaminio na hakuna kinachosimama kati yako na Mungu unaweza kuomba chochote utakacho na unajua kuwa utapewa, kwa sababu ni Neno ambalo wewe umepewa ilivyo kuwa kwa wale wanafunzi ***(Yohana 14:13).***

Sasa jambo pekee upaswalo kufanya sasa, kuwa na imani kwa kila ulichokuwa. Na imani kwa lile Neno unachosema wewe ni nani? Na Yesu alikuwa na imani katika Neno la Mungu,lililosema kile alichokuwa."Imeandikwa juu ya imani"Je Daudi katika zaburi na manabii na sehemu zote hawakuzungumza juu ya Yeye? (luka 24:27)"Mimi ni mkate wa uzima utokao kwa Mungu huko mbinguni"[yoh 6:33-35;48-51] Amen!"mimi ni mti ule wa uzima"
***[Mwanzo 2:9; 3:24]*** kutoka bustani ya edeni, mimi ni hivi vitu vyoye.**MIMI NIKO AMBAYE NIKO** ***[Kutoka 3:: 13-15]*** Na alijua na ile kamilifu,kwamba yeye ni mpakwa mafuta mesiya, Na kwamba Roho wa Mungu alikuwa juu yake. ***(Luka 4:14-21, Isaya 61:1-3; Yoh 4:25-26)*** Alisema"sasa mimi mwenyewe siwezi kufanya lolote; Lakini ni imani yangu katika Mungu,na kwamba Mungu alikuwa ndani yake. Neno limedhihirishshwa na Neno la Mungu linapo kuja ndani yake, linadhihirishwa,kwa maana wewe ni mwaminio.Unaona na mwaminio"Imani ya Mungu ambayo inatenda ndani yako" ***(2Kor. 4:13;Galatia 2:19-20;Mark 11:22).*** Ninapenda kufundisha juu ya imani hasa ni nini ***(Wabr.11:1).***
Akijijua yeye ni nani bila kivuli cha shaka yoyote, Akijua Yeye ni mwana wa Mungu, alifahamu hilo kwa maana lile Neno lilijitambulisha. Neno la Mungu lilitambulisha Yeye alikuwa nani

alisema,"kama sizitendi kazi za baba yangu,msiniamini,lakini nikizitenda ,japokuwa hamniamini mimi,ziaminini zile kazi ***(Yohana 10:37-38]*** Lakini kama ninazifanya,basi aminini hiyo kazi,kwa maana ni Neno lililo ahidiwa lili jidhihirisha,oh kama tu ungeamshwa katika Roho,kwa dakika! Unaona, Neno lenyewe lilimtambulisha Yeye,Alikuwa nani,alikuwa [Isaya 7:14; ***isaya9:6-7; Isaya 42:1-4;Isaya 53:2-12;Mwanzo 49:10; Hesabu 24:17; zaburi 16:9; Isaya 9:1-2 [mathayo 4:12-17] Isaya 50:6; Zakaria 12:10; Zaburi 34:20; Zakaria 9:9 [Luka 19:28-38] Kumbukumbu 18:15-18…..*** Akasema "Naniawezaye Mimi kwamba nina dhambi? Kwa maneno mengine"Ninani awezaye kunionyesha Mimi kuwa maisha yangu ni kazi yangu havitimizi hasa vile mesiya aposwayo kufanya?" Hakuna ambaye angesema chochote maana alikuwa ndiye,Hapo sasa alikuwa na imani ya kuamini;chochote kile ambacho alisema kingetokea. [1]

Alikuwa ni udhihirisho wa Neno kwa wakati ule alikuwa (Isaya9:6)" kwa ajili yetu mtoto amezaliwa" na kadhalika pia alikuwa pia (isaya 35, isaya 28:19), yuleyule hizi, haya maandiko yote yalikuwa yametabiriwa kimbele, alikuja kulidhihirisha hilo neno, alifanya kile kinachopaswa kufanya katika siku ile. Kwa maana neno hili, kitabu ni neno La Mungu na neno ni Mungu. [2]

Kwa maana neno limetambulisha limejitambulisha lenyewe, kile alichokuwa , na neno hilihilo linatutambulisha sisi. [1]

***(Ufunuo 10:8-11, 1Yoh 3:14, 1Yoh 4:7-8, 1Yoh 5:1-4, 18-20, Mathayo 5:43-48, Marko 16-18, Galatia 4:6, Waebr 10:1-2, Yoh 7:37-39, Yoh 10:26-30, Yoh 17:6-10, Rumi 5:1-5, Rumi 6:6-11, Rumi 7:1-6, Rumi 8:1, 11,14-17, 1kor 13:1-3, 2kor 5:14-15, Galatia 2:20, Efeso 1:13-14, Waebr 4:1-11) Etc.***

Unaona? "Kama mtu akinipenda mimi atazishika amri zangu, na kama anasema ananipenda mimi na hazishiki amri zangu (yaani amri zote) yeye ni mwongo, na kweli haimo ndani yake" ***(1Yoh:2:3-6, Yoh 14:21).***

Unasema "Vema siamini lolote ………." Vema sasa wewe ni asiyeamini tu, ndiyo hivyo. Kama Biblia ilisema hivyo, hiyo inalifanya kuwa ni sahihi, hiyo inakuwa hivyo milele, vile Biblia inavyosema ndiyo kweli.

Sasa, angalia alijua yeye ni nani, kwa hiyo alikuwa na imani, imani ingezaa wakati alipotambua yeye nalikuwa nani "kama mkikaa ndani yangu na maneno yangu ndani yenu". "hapo sasa mnajua ninyi ni nani" omba utakalo na utalipokea***" (Yoh 15:7)***

Je hilo halitakuwa la ajabu? Kama kila mmoja anayekuja kwenye ule mstari wa maombi anasema "mimi ni mkristo, sina hukumu katika dhamiri yangu, ninajua dhamiri yangu hainihukumu, kitu flani kinaniambia huu ni mwisho wa mateso yangu" kile unachoenda kufanya, utaenda zako hapa ukiwa na kitu fulani, haijalishi unakuja na misisimko mingapi, kiasi gani

utafanya, haitafanya kazi mpaka uje na ile imani kamilifu iliyojitambulisha yenyewe ndani yako, kama kitu halisi. Na inapokuwa iko pale, hapo sasa hakuna kitu kitakachokutikisa kuacha hiyo!

Kama ungekuwa na kansa, na daktari amekuambia jana utaenda kufa kabla ya asubuhi ifuatayo ( moyo wako wote, mapafu yako yote yamekwisha, kansa imekumaliza, damu yako yote ni kansa, chochote kiwacho) na kitu Fulani kinakuja na hii imani halisi ya hakika, imani kamilifu imefanywa kuwa kitu halisi ndani yako, ungeweza kumcheka yule Daktari asemacho.
Yesu alikuwa na imani kamilifu, alikuwa nayo, imekuja kwake kwa sababu yeye alikuwa neno, na wewe unakuwa neno; unakuwa neno kwa kadiri unavyolipokea neno " kama mkikaa ndani yangu na maneno yangu yakakaa ndani yenu, maneno yangu ambayo………(hili neno) likiwa ndani yenu ombeni mtakalo nalo litaffanyika, unaona? Kama utauambia mti huu ng'oka na usione shaka, nawe uamini juu ya kile ulichosema, hapo utapata kile ulichokiomba. Mnapoomba amininі kuwa mnapokea yale mliyoomba, utapewa hilo ***(Marko 11:23-24)*** Wakati, nafasi, hakuna chochote kiwezacho kubadilisha hilo unajua limefanyika, hilo linakuwa limemalizika.

Sasa , angalia; sasa na alituambia sisi. "kama mkikaa ndani nyangu na maneno yangu ndani yenu" Yohana Mtakatifu hapa " mnaweza kuomba lolote mtakalo, mtatendewa" (***Yohana 15:7).*** Hapo sasa tambua nafasi yako katika maandiko kama mwaminio (***1wathesalonike 1:4-6)*** unaona, unapaswa kutambua nafasi yako.

Sasa unapaswa kuamini kile unachokiomba kama wewe ni mwamini, jitambue mwenyewe kama mwamini, tambua ya kuwa haya mambo ni kwa ajili yako.

Kama dhamiri inakushtaki katika maisha yako, rekebisha hilo kwanza. Unaona? Kama dhamiri inakushtaki unaweza ukawa na watu zaidi ya dazeni ambao wanayo imani ya kuja hapa na kukuombea wewe, na kuruka juu na chini na kukumwagia wewe galoni kwa galoni. Haitaondoka. Hiyo ni kweli,

Nenda karekebishe, kasahihishe hilo jambo. Nenda ukatubu dhambi hiyo kwa mume wako, kwa mke wako. Nenda fanya jambo hilo. Haitakufanyia jambo zuri kamwe, haijalishi unaomba kwa nani, mpaka ulisahihishe hilo moyoni mwako dhamiri inakushitaki. Na Mungu hatakuja katika moyo huo ulio na hukumu. Unaona? Mungu hakai katika huo, unapaswa ulisahihishe hilo sasa. Unapofanya hivyo inabidi uwe na imani kama kila kitu kimesahihishwa inabidi uwe na imani kuamini hilo usiogope.

Katika kitabu cha Ayubu kinasema hapo. "Ayubu aiogopa" na kile nalichoogopa ndio hasa kilichotokea, ni kitu gani kilicholeta hilo? Hofu yake ***(Ayubu 3:25)*** hiyo ndiyo iliyofanya likatokea. Imani yake ingeweza kumuweka mbali na hilo. Lakini wasiwasi wake ulimfanya alipate hilo, aliogopa kwamba hilo lingetokea na likatokea. Na sasa kama angejua halitatokea lisingetokea, unaona ninachomaanisha? [1]

Angalia uone mwaminio aabudiye alitambulishwa na sadaka yake kwa ile ishara. Mwabudu ambaye alimwamini Jehova, na anayeweza kufanya yote anayohitajika na Jehova,

amejitambulisha mwenyewe kwa kupata ile ishara kwake yeye mwenyewe na nyumba yake. Hivyo alikuwa ni mwabudu anayeamini hilo***.(Kutoka 12:1-3)*** huo ni mfano Mtakatifu wa Kristo katika siku hii ya leo;l halafu ile damu ilikuwa ni ishara ya utambulisho kwamba huyu mwamini amefanya yote yaliyotakiwa na jehova. "Na nina uhakika Yule malaika muuaji atapita nyumba yangu kwasababu nimefanya yote yaliyo takiwa kwa ishara ile ya Jehova.Mwanakondoo amekufa kibadala kwa ajili ya nyumba yangu na wapendwa wangu walio chini ya damu;Hapo sasa ipo ishara kuwa mwanakondoo amekufa "Amina", "hiyo hapo ile ishara. Mahitaji yaliyohitajika na Mungu yametoshelezwa. "amina" ninapofikiria juu ya hilo moyo wangu unaruka kwa furaha.

Sasa tunayo ishara katika siku hii ya leo, tumepewa ishara ambayo ni kitu halisi cha kielelezo cha ile ishara ya kimwili. Tumepewa ishara kuu ya kimiujiza, vitu ambavyo vilielezwa. Huko nyuma tumepewa katika hiki kizazi. Sisi tumepewa ile ishara. Sasa tunaye Roho Mtakatifu ndiye ishara yetu na kitambulisho chetu kwamba tumekubali kifo cha mwanakondoo. Sio kwamba Yesu alikuwa uhai tu wa kibinadamu uliokuja kwetu tena, lakini alikuwa ni Mungu mwenyewe akidhihirishwa katika mwili, ambayo hiyo ilileta kwetu hali ya kufanywa wana, kwamba sisi ni wana na binti wa Mungu. Hiyo ndiyo ishara, ni kitambulisho chetu cha pasaka, ni kitambulisho chetu kwamba tumemwamini Mungu na Mungu ametukubali.

Pale nyuma hawakuwa na injili kama tuliyonayo leo, walifundishwa kwa namna ya mifano na ilifanyika kwa taratibu kwa sababu Roho Mtakatifu alikuwa hajatolewa, lakini leo tuna kitu halisi, hatuna vitu vya mfano au vitu vya kikemia, kwa sababu usingechukua damu ya Kristo uipake kwa kila mtu. Na hicho ndiyo kitambulisho chako kwamba umekubali mpango wa Mungu na kwamba umefanya yote aliyotaka Jehova. Ambayo alifanya kwa ajili yako pale kalvari na wewe umefanya hayo yote Katika magoti yako na mungu amekupa wewe ile alama ya ishara kwa kumtuma roho mtakatifu aliyekuwa juu kristo ambaye yuko ndani yako na uhakika wa utambulisho .wa uhai wake kifo kuzikwa na kukufufuka na kwamba yuko hai milele na milele katika kanisa la waloamini aimina ni ishara halisi alama ya ishara .

Sasa damu iliyomwagika pale msalabani ikamwagika ardhini na tuna ishara ya damu ambayo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu kututambulisha sisi kama waminiio ***(Waefeso 1:13-14) (2wakorinto Marko 16 : 17 -18)*** siyo tu kukiri lakini ni kitambulisho cha muaminio wanaweza wasifuate pengine wanafuata au labda wata? Yesu alisema zitafuatana na hao waaminio ni jambo la uhakika haiwezekani ulitokee kazi nizifanyazo mimi nanyi mtazifanya pia(***Yohana14:12***) hilo ndilo kitambulisho kitambulisho cha yesu kilikuwa ni kudhihilisha neno la mungu ambaye yeye alikuwa neno na kitambulisho cha kanisa leo ni kudhihirisha ahadi za neno la Mungu kwa siku hii ya leo kwa Roho yuleyule aliye analihuisha neno wakati huo. Roho yuleyule analihuisha neno kwa muaminio leo na kudhihirisha jambo lile lile . kuonyesha kwamba ile ishara iko juu ya ya huyu mtu .Ambayo uhai ya ufufuo wa Yesu Kristo ukiishi ndani ya waaminio wake . ooh hilo unapaswa kuliweka kanisa katika moto? na hiyo ni kweli kama kweli

inavyoweza kua. Inabidi tujitambulishe wenye sadaka yetu inabidi tutambulishwe na kifo chake wakati myahudi atakaweka mikono yake juu ya sadaka yake alikuwa anajitambulisha yeye mwenyewe akihamisha dhambi zake kuweka kwenye sadaka yake na ile sadaka ilikufa .na sasa tunaweka mikono yetu kwa imani juu ya Yesu kristo na tunatambulishwa na yeye katika mauti yake siyo tu katika mauti yake lakini kama tumekubalika hatutamulishwi tu katika mauti yake bali katika kufufuka (Warumi6:3-5).kwa maisha yale yaliyokuwa ndani yake yanarudishwa tena kwa muaminio kama ishara kwamba kukumbuka kwamba imepita juu yake na kwamba Mungu amekutia muhuri katika ufalme wake mpaka siku ya ukombozi ***(Waefeso4;-30)*** Ile Injili halisi kabisa safi kama ninavyojua yaani hiyo najua ni kweli nimelijaribu hilo hakuna uzushi wowote hakuna msisimko wowote hilahila zozote .hapana hakuna hiya ni imani safi isiyoghashiwa katika neno la Mungu . Na kazi iliyomalizika ambayo Mungu alihifadhi pale kaloari.tukijua kwamba hakuna chochote tungeweza kufanya kujiokoa wenyewe .tumekubali tu kile ametufanyia siiiblahimu alimuamini mungu ikahesabiwa kwake kuwa haki halafu mungu akampa yeye muhuri ya tohara ***(Warumi 4:11-12 )***kuwa kama ishara kwamba imkubali imani yake hiyo hapo Injili
Sasa tunapodai kwamba tunamuamini Mungu nae ataitambulisha imani yetu kwa kutupa ishara ya damu ya Yesu ambayo uimaliza kazi kwa ajili yetu pale msalabani hapo sasa uhai wetu uko ndani yake. Uhai wa sadaka yetu uko dani yetu.

Lakini sasa ule uhai uliokuwa ndani ya damu unakuwa ile ishara, na sasa tunapojitambulisha sisi wenyewe katika kifo chake, kuzikwa kwake, kufufuka kwake kwa kumuamini yeye, kwa kubatizwa kwa kufa kwake, kuzikwa kwake na kufufuka kwake (warumi 6:3-5) tunapoinuka juu Roho Mtakatifu yuko pale kutupa sisi ile ishara, ishara ya milele iliyoandikwa katika mioyo yetu, nafsi, utu wako, maumbile yako, akili yako,( nia yako) mwili wako na kila kitu. Kwamba wewe ni mtu uliyetengwa kutoka kutokuamini, wewe ni mtu uliyetengwa na mambo ya ulimwengu. Umetengwa kutokana na mauti kutokana na kila kitu, na wewe ni zao la Mungu ambalo limetiwa muhuri katika ule ufalme kwa Roho Mtakatifu. Hakuna shetani, hakuna magonjwa hakuna kifo, hakuna huzuni au kitu chochote kinachoweza kukusumbua wewe ilimradi uwe unashikilia ile ishara katika jambo hilo. Amen. Imani yako isiyibadilika inadunda hivyo na inaunda mfano wa Yesu Kristo katika sura ambayo unatembelea leo na ni nionapo ila damu “nitapita juu yako” ***(Kutoka 12:13)*** hiyo ni ishara ya kwamba gharama imelipwa, Yesu amelipa gharama na wewe unaipokea hiyo kutoka unaposhikilia ile ishara mkononi mwako, unakuwa na uhakika wa ufunuo. Na una uhakika kwamba kila kitu unachokihitaji katika safari yako umepewa katika ishara ya mateso yake pale msalabani mahali ambapo aligharimia na kulipa gharama ya kila laana ambayo ingewekwa juu yako. Ile ishara inazungumzia amani, hakuna pepo linaloweza simama mbele yake, hakuna pepo anayeweza kusimama mbele yake wala hakuna chochote kinachoweza kusimama mbele yake kwa sababu Mungu ameikubali hiyo na wewe unaishikilia ile ishara mkononi mwako kwamba gharama imelipwa, Ooh! Ni ishara chanya/halisi [2]

Na sasa Kristo alikuwa mwanakondoo mkamilifu ***(Yohana 1:29),*** sasa kupitia kumwagwa kwa damu ya huyu mwanakondoo, sasa Yule mwanakondoo wa asili kule Misri, ile damu yake ilipopakwa, walipoiweka ilisimama kama ishara. Hapo sasa damu ya mwanakondoo ilisimama kwa ajili ya nini? Unaona? Ile ishara ilimaanisha kwamba tumekufa sisi wenyewe na tumejitambulisha na ile sadaka ***(Warumi 6:6-11***) unaona? Sasa yule Mwanakondoo, ile damu ya Yule mtu vinatambulishwa pamoja, ile sadaka ya mwaminio. Unaona? Unatambulishwa katika maisha yako kwa sadaka yako, hiyo kukuwezesha wewe kuwa kile ulicho.

Sasa hiyo damu ilikuwa ni ishara au ilikuwa ni kitambulisho, ile damu ilimtambulisha mwabuduo kwamba amemchinja mwanakondoo na amemkubali mwanakondoo na akaipakaa ile ishara kwake yeye mwenyewe kwamba haionei haya. Hakujali ni nani anaiona hiyo alitaka kila mtu aione hiyo na aliweka katika mahali ambapo kila mtu anayepita aliweza kuiona ile ishara.

Unaona, watu wengi wanataka kuwa waKristo, wanataka uKristo wao kuwa wa siri, ili kwamba hakuna mtu anayejua kwamba ni waKristo au marafiki zao wanaotembea nao, sasa unaona huo si uKristo, uKristo inabidi uonyeshe ishara yako na uionyeshe hadharani, uionyeshe waziwazi kule ofisini, kule barabarani, unapokuwa na matatizo yanayokuzunguka, au chochote ikiwa ni kanisani au chochote kile. Ile damu ni ishara na inabidi ipakwe vinginevyo lile agano halina nguvu.Ile damu ilikuwa ishara au ilikuwa kitambulisho kwamba huyu mtu ameokolewa. [3]

Ni ushahidi gani unaonyesha mtu amejazwa hasa na Roho mtakatifu? "Roho Mtakatifu anapokuja atakuonyesha mambo yajayo" ***(Yohana 16:13-14)*** unaona? Ataikamilisha hiyo, vitu vilivyotengenezwa na watu haviwezi kufanya hivyo, na yeye ni neno. Yeye Roho Mtakatifu atakapokuja atajitambulisha ndani yako na maandiko, yeye mwenyewe, na hiyo ni ishara ya kweli kwamba. Roho mtakatifu yuko ndani yako kwa sababu yeye ni neno. [4]

Na tunapongalia katika neno la Mungu hebu tujitambulishe sisi wenyewe kwa maana aliwatoa watu wengine kwa mfano wetu vile tulivyo. Kwa hiyo hebu tuangalie sasa kama tunaweza kujitambulisha hali yetu ua sasa pamoja na watu wa Biblia. [5]

Unaweza ukajitambulisha wewe mwenyewe mahali popote unapotaka katika maandiko kama wewe ni mkristo. [6]

Sasa hebu tuangalie katika kioo cha Mungu Neno Lake. ***(Yakobo 1:22-25)*** na kajitambulisha hali yetu ya sasa na tabia za kwenye Biblia. Jitambulishe wewe mwenyewe, hebu tuangalie katika hii na kuona kama tunaweza kujiona sisi wenyewe kupitia tabia za watu katika Biblia tuone walifanya nini katika mazingira flani, na kuona tunafanya nini sasa. Sasa unifate mimika karibu sasa, angalia tabia ya sasa kama ilivyo mKristo, sasa unaweza kujihukumu, hilo halimfanyi mtu yoyote akuhukumu wewe , unajihukumu mwenyewe ***(1Wakorintho 11:31)*** hakuna anayekuhukumu wewe, mimi sitoi hukumu, lakini hebu tuangalie tuone tunaonekanaje na baadhi ya tabia za Biblia kadri tunavyozitaja hizo, na kuona tabia yako ikoje katika wakati huu tulionao,

sasa angalia lile neno Linaumba tabia tunajua hilo, sasa hebu tuangalie katika kioo na kujitambulisha sisi wenyewe na watu Fulani katika Biblia. [5]

Jambo hilohilo kwa kuwa Mkristo wa kweli ni lazima utambulishwe na hilo, nilihubiri pamoja na nuru na kuwaonya watu juu ya hukumu inayokuja, hiyo ni kounyesha kuwa mKristo halisi, nilikuwa na Musa katika kichaka kile kinachowaka moto nikaiona ile nguzo ya moto na nikauona utukufu wake, nilikuwa na Musa kule jangwani, ili uwe mKrist inabidi nitambulishwe na kila kitu alicho Mungu ili kuwa mKristo. Nimeuona utukufu wake na nimesikia sauti yake, usijaribu kunieleweesha kinyume na hilo sasa. Kwa sababu nilikuwa palena ninajua kile ninachokizungumzia, nimeona lililotokea, ndiyo bwana. [7]

Mungu yu ndani ya mtu na anajitabulisha yeye mwenyewe leo ndani ya kanisa lake, katika mKristo aliyezaliwa mara ya pili. Mungu anajitambulisha. Mungu anajitambulisha mwenyewe na anabakia kuwa ni Mungu na ulimwengu wanje unamjua Mungu kadiri wanavyomuona Mungu ndani yako wewe na mimi. Hiyo ndiyo njia ya pekee watakayomjua Mungu, ni sisi tunapokuwa barua zilizondikwa na maandiko, tunasomwa na watu wote ***(2Korintho 3:2-3)*** na maisha ambayo tuaishi yanaonyesha kilicho ndani yetu, mtu hutambulishwa na kazi anazozitenda, kwa hiyo kazi zetu siku zote ziwe nzuri. Unaona? Siku zote ziwe nzuri, kwa sababu tunamwakilisha bwana wetu Yesu Kristo. [8]

Na leo anasimama miongoni mwetu katika utu wa Roho Mtakatifu, akijidhihirisha yeye mwenyewe zaidi na zaidi, akija ndani ya kanisa lake, akijitambulisha yeye mwenyewe, kwa sababu yeye, na bibi harusi na bwana harusi watakuwa sawa, akjitambulisha yeye mwenyewe. Siku moja utamuona Yule ambaye ulimsikia moyoni mwako na kuona utambulisho wake, utaumbika katika utu mbele yako, hapo sasa wewe na yeye ni mtu mmoja na mmeungana kwa njia ya neno. hapo mwanzo neno lilikuwepo litaenda kule nyuma mwazoni ambako lilikuwa ni Mungu “na siku hiyo mtatambua kwamba ni ndani ya baba na baba ndani ya mimi na mimi ndani yenu na baba ndani yenu***”(Yohana 14:20)*** haleluya! Tuko hapa. Ninayo furaha sana kumuona yeye akidhihirishwa mwenyewe miongoni mwetu na kuona kile alichokiahidi kwenye neno lake, siyo msisimko flani kuimba, kurukaruka na kucheza, lakini kwa neno lake. Amejifanya yeye mwenyewe ajulikane. [9]

Na tuko hapa wakati wa laodikia wakati wa usodoma na ile huduma imekuja kupitia kila kona ya neno la Mungu na ninaamini siri yote ya Mungu imekwisha hubiriwa na sasa inatambulishwa kwamba ni Kristo miongoni mwa watu wake, Mungu akitenda kazi kupitia miili ya kibinadamu. ***(Yohana 2:7)*** [10]

**NUKUU ZA KIINGEREZA**

[1]Imani kamilifu (63-0825E)aya 64-70,74-79,93-94,95-98,101-102

[2]Ile ishara(63-1128E)aya 26 ,47-63

[3]ishara(63-0901m)aya 67-71

[4]maswali na majibu(64-0823E)

[5]kitambulisho(64-0216)aya27,91-92

[6]maswali na majibu(64-0830m)GOD ukurasa 1104 Aya197

[7]mungu mkuu akifunuliwa mbele yetu (64-0629)Aya 189-191

[8]shalom(64-0112)AYa ya 9

[9]kujaribu kumtendea mungu kazi bila mapenzi yake (65-6718m)Aya 174

[10]yesu kristo Yule jana leo hata milele(63-0627)Aya 247

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 15 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii, Yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr. 69 D-75328 Schomberg, Germany Simu (+49) 72357613 Fax: (+49) 72353306

---

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu iliyokusudiwa kimbele imesikia.

(Ndugu Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho uk 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju.*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*